

Falcon

ULEAJI WA VIFARANGA

Kimetayarishwa na:
FALCON ANIMAL FEEDS LTD.

INTRODUCTION

Falcon Animal Feeds Ltd ni kampuni inayojihusisha na uzalishaji, usambazaji wa chakula cha kuku pamoja na uzalishaji wa vifaranga (Happy Chicks).

Pia tunatoa huduma za ushauri wa kitaalamu kwa wafugaji pamoja na namna bora ya ufugaji kwa kutumia wataalamu wetu ambao ni wabobezi kwenye maswala ya kuku na mifugo mingine.

Falcon Animal Feeds Ltd inatoa huduma zake katika mikoa yote ya Tanzania bara na visiwani.

Kampuni pia kupitia huduma zake inakuhakikishia mdau na mteja wa falcon kupata yafuatayo wakati wote:-

- Upatikanaji wa chakula wakati wote.
- Huduma za wataalamu wetu.
- Kupokea maoni na ushauri kutoka kwa wafugaji na mawakala.
- Kuzalisha vyakula vyenye ubora wa hali ya juu.
- Kushirikiana kikamilifu katika changamoto zinajitokeza kwa mawakala wetu na wafugaji.

ULEAJI WA VIFARANGA VYA KUKU

Vifaranga wenye umri wa kuanzia siku moja wanahitaji uangalizi wa hali ya juu kutokana na mahitaji yao ikilinganishwa na uwezo wao mdogo wa kuzalisha joto katika miili yao.

Katika uleaji wa vifaranga ni muhimu kuzingatia

1. Maandalizi ya Banda

Banda linatikiwa kuandaliwa wiki mbili kabla ya kupokea vifaranga. Maandalizi hayo huambatana na usafi pamoja na upuliziaji wa dawa ya kuua vimelea vya magonjwa nje na ndani ya banda.

Samabaza chokaa katika banda na siyo kupaka kama rangi. Pia wakati wa kuandaa banda inaendana sambasamba na utengenezaji wa sehemu ya kulelea vifaranga (Brooder) kipindi cha siku za mwanzo wakati wakipatiwa joto.

Hakikisha vyanzo vya joto vinaandaliwa na pia unafunga taa kwa ajili ya mwanga.

Mchoro: Namna unaweza kutenga sehemu ya banda kwa ajili ya kulelea vifaranga

2. Uwekaji wa Maranda (Litter requirement)

Maranda yana umuhimu mkubwa katika ufugaji wa kuku kwa jumla.

A. Umuhimu wa Maranda kwenye banda;

i/. Kutunza joto ndani ya banda

ii/. Kufyonza unyevu kwenye banda.

Maranda ya aina mbalimbali yanaweza kutumika hasa ikizingatiwa upatikanaji wake katika maeneo husika.

Mfano wa Maranda na kiasi kinachohitajika kuwekwa kwenye banda.

AINA YA MARANDA	KIWANGO
Maranda makavu ya mbao (makubwa) (Dry sawdust)	Kuanzia 2.5cm
Maganda ya mchele (Rice Hulls)	Kuanzia 5cm

- Kwa kutumia kidole unaweza kupima kiwango cha Maranda kinachohitajika, kwa kuzingatia kina chake.

- Pia kama maranda yatawekwa katika banda ambalo halijasakafiwa kiwango cha Maranda kinatakiwa kuongezeka Zaidi, kuanzia sentimita 10.

- Kwa watumiaji wa Maranda ya mbao wanafaida Zaidi kwani yanauwezo mkubwa kufyonza unyevu, ila tumia Maranda yenye saizi kubwa sio ya vumbi.

- Weka Maranda mengi ili uwe unayageuza mara kwa mara nasiyo kubadilisha kwa kipindi kirefu.

3. Uingizaji hewa (Ventilation)

Katika kipindi cha uleaji wa vifaranga hakikisha banda linaingiza hewa safi na toshelezi. Ukuaji mzuri wa vifaranga hutegemea hewa safi na inayotosha. Epuka kujenga banda lako sehemu yenye muelekeo wa upepo.

4. Uwekaji wa Magazeti

Kabla ya kuwapokea vifaranga ni muhimu kutandaza magazeti juu ya maranda katika sehemu ya kulelea vifaranga (Brooder).

Faida za kutumia magazeti;

i. Hurahisisha vifaranga kutembea ili kufuata chakula na maji.

ii. Magazeti husaidia vifaranga kula chakula kwani kipindi vifaranga wanadonoa chakula kwenye magazeti ule mlio au sauti huhamisisha na vifaranga wengine kuiga na kula, hivyo hupelekea ukuaji mzuri wa kuku.

iii. Huzuia ulaji wa maranda na kuwafanya kuzingatia ulaji wa chakula ndani ya siku tatu.

iv. Magazeti yawekwe asilimia hamsini tu ya sehemu iliyotengwa kulelea vifaranga.

v. Pia waweza tumia sahani au sinia kama mbadala wa magazeti.

5. Idadi wiani ya vifaranga katika banda

(Stocking Density)

Idadi yavifaranga unaowachukua ni muhimu kuzingatia kulinganisha na ukubwa wa banda lako. Pia kumbuka kua kadri kuku wanavyoongezeka uzito ndio wanahitaji nafasi kubwa zaidi.

Jedwali: *Umri wa vifaranga na mahitaji ya nafasi katika sehemu ya kulelea vifaranga (Brooder).*

UMRI WA VIFARANGA (SIKU)	IDADI KWA M^2
0 - 3	55 - 60
4 - 6	40 - 45
7 - 9	30 - 35
10 - 12	20 - 25
13 - 15	10 - 15
16 -	8 - 10

Ili kupata matokeo mazuri katika ukuaji wa kuku wako hakikisha una wapatia nafasi ya kutosha.

Zingatia uongezaji wa nafasi ya chumba ulichofungia vifaranga (Brooder) kadri umri unapoongezeka.

6. Joto

Katika kipindi cha uleaji wa vifaranga, joto ni sehemu ya mahitaji muhimu ya kifaranga. Hii ni kutokana na kutokuwa na uwezo wa kuzalisha joto la mwili.

Mahitaji ya joto kwa kifaranga wa siku moja (Day old chick) hutofautiana kutokana na maeneo tofauti kulingana na joto ridi iliyopo na unyevu unyevu katika hewa (Humidity).

Hivyo ni muhimu kuzingatia kuwapatia joto vifaranga mpaka kipindi wakiwa na uwezo wa kuzalisha na kutunza joto katika miili yao, na hili huangaliwa kwa kiwango cha manyonya.

Pia vyanzo mbalimbali vinaweza kutumika katika kuhakikisha upatikanaji wa joto;

i. Gesi
ii. Umeme (Bulb)
iii. Mkaa (Majiko ya mkaa au Vyungu).

Vyanzo hivi hutumika kulingana na mahitaji na upatikanaji katika maeneo husika. Ili kuhakikisha kiwango cha joto linalohitajika kinapatikana, huwa ni vizuri kuziba madirisha kwa sehemu kubwa kwa siku za mwanzo (1-3) na kuondoa baada ya siku hizo pia ukizingatia na hali ya hewa.

Kiwango cha nyuzi joto kinachohitajika kuanzia siku ya kwanza mpaka ya 14 katika maeneo ya joto na hali ya juu ya unyevu katika hewa (Humidity).

Mfano wa mikoa; Dar es salaam, Tanga, Morogoro, Lindi, Mtwara, Visiwa vya Zanzibar

UMRI (SIKU)	NYUZI JOTO
1	31°C
2 - 3	29°C
4 - 6	28°C
7 - 14	25°C

Katika mazingira ya joto kama Dar es Salaam si lazima kutumia vyanzo vya joto kutokana na kuwa na joto linalojitosheleza.

Kwa maeneo yenye kiasi kidogo cha unyevu unyevu hewani na kiwango cha chini cha nyuzi joto kama; Iringa, Njombe, Mbeya, Arusha, Kilimanjaro.

UMRI (SIKU)	NYUZI JOTO
1	35°C (34°C)
2 - 3	31°C
4 - 6	27°C
7 - 14	21°C

Wakati wa kuwawekea joto vifaranga ni vizuri kuweka kipima joto (Thermometer) bandani ili iwe rahisi kutambua hali ya joto.

Hakikisha katika siku za mwanzo za uleaji wa vifaranga mhudumu anakua karibu ili kuhakikisha vifaranga wanapata chakula na maji wakati wote na kuhakikisha joto toshelezi.

7. Mahitaji ya Chakula

Chakula ni sehemu mojawapo muhimu ya kuzingatia katika ufugaji. Baada tu ya kupokea vifaranga na kuviweka katika sehemu ya kuwalelea (Bruda) hakikisha unawawekea chakula katika sahani au magazeti.

Chakula bora ndio mwanzo bora wa kupata kuku wazuri na wenye uzito mzuri katika kipindi cha kuwauza.

Hakikisha vifaranga wamekula chakula angalau ndani ya masaa manne baada ya kuwaweka katika bruda.

Kwa mtumiaji wa chakula bora kutoka Falcon Animal Feeds Ltd. Zingatia matumizi sahihi ya chakula kama ifuatavyo:-

Kwa kuku wa nyama.

Starter Crumble
Tumia mfuko 1 (50kgs) kuku 100.

Grower Crumble
Tumia mfuko 1 (50kgs) kuku 100.

Finisher Pullet
Tumia mifuko 2 (100kgs) kuku 100.

Post Finisher
Tumia kuanzia siku ya 29 - 42, utapata uzito kuanzia 2.5kgs -2.8kgs.

Katika Kipindi cha uleaji Vifaranga fuatisha michoro hapo chini:-

	• Muonekano wa Vifaranga wanaopata joto linalotakiwa. • Huwa wachangamfu na Kusambaa.
	• Muonekano wa Vifaranga kutokana na upungufu wa joto. • Vifaranga wanajikusanya na kusogelea chanzo cha joto.
	• Muonekano wa Vifaranga kutokana na kuzidi kiwango cha Joto. • Vifaranga hukaa mbali na chanzo cha Joto.
	• Muonekano wa Vifaranga waliorundikana upande wa Bruda usifikiwa na Upepo.

Falcon

Wasiliana nasi:-

+255 677 531 010
marketing@faf.co.tz
Falcon_animal_feeds_ltd
Falcon_happychicksTanzania
Falcon_ animalfeeds_Tanzania
Falcon_animal_feed_Tanzania
www.faf.co.tz